

## MPANGO WA KURUDI TENA SHULENI WA VIKTORIA

| Vitendo muhimu   | 1: Wanafunzi wa P-2 na Sekondari Kubwa warudi tena kwa mahali pa shuleni  | 2: Wanafunzi wote warudi kwa mahali pa shuleni, wiki mbili baadaye   | Shughuli za shule za kila mara zianze tena kufuata mashauri ya afya  |
|--|---|--|--|
| <ul style="list-style-type: none"> <li><b>Kusafisha</b><br/>Shule zitasaidiwa kutekeleza usafishaji ziada, ikiwa pamoja na kusafisha kote siku kwa nyuso za kuguswa sana kama vyumba vya bafu na vipete vya milango.</li> <li><b>Kuweka umbali wa mwili</b><br/>Wafanyakazi wote wa shule watasaidiwa kuweka umbali wa mwili, lakini umbali wa mwili hapimwi lazima kati ya wanafunzi kwa mahali pa shule.</li> <li><b>Usafi</b><br/>Kuosha mikono mara nyingi kutahimizwa kati ya wafanyakazi na wanafunzi na, ambapo sabuni na maji hayapatikani, dawa yenye alkoholi ya kusafisha mikono itatumika.</li> <li><b>Afya</b><br/>Yeyote anayehisi mgonjwa asihudhurie shuleni, ikiwa pamoja na wafanyakazi, wazazi na wanafunzi.</li> </ul> | <p><b>Wanafunzi wa (Prep – 2) na Sekondari Kubwa (Mwaka 11 na 12)</b><br/>Wanafunzi wa Prep hadi Darasa la 2 na wanafunzi wa Mwaka 11 na 12 watarudi kwa mahali pa shule kwanza. Programu iliyopo ya kujifunza kwa mbali haitaendelea kwa wale wa miaka hii.</p> <p><b>Wanafunzi wa Darasa la 3 – Mwaka 10</b><br/>Wanafunzi wa Darasa la 3 hadi Mwaka 10 wanaoweza kujifunza nyumbani wanapaswa kuendelea kujifunza nyumbani. Wanafunzi hawa wataendelea kusaidiwa na shule yao kujifunza kwa mbali.</p> <p>Wanafunzi ambao hawawezi kujifunza nyumbani wanaweza kuendelea kuhudhuria programu ya kusimamishwa kwa shule zao.</p> <p><b>Wafanyakazi wa shule</b><br/>Wakati wa Hatua ya Moja wafanyakazi wote wa shule wanatarajiwa kuwepo eneo la shule.</p> <p>Wafanyakazi watasaidiwa kutunza ustawi wao kupitia shule zao na Programu ya Msaada wa Wafanyakazi.</p> <p><b>Wazazi</b><br/>Wazazi wafuate mashauri kutoka shule yao kuhusu protokali za kuacha na kuchukua watoto.</p> | <p><b>Wanafunzi wote warudi kwa mahali pa shule</b><br/>Wanafunzi wa miaka yote watarudi shuleni.</p> <p>Shughuli kama kambi, safari na kutembelea hazitatokea hadi vizuizi vya usafiri vya sasa vitaondolewa.</p> <p>Shule hazitatoa tena programu ya kujifunza kwa umbali.</p> <p><b>Wafanyakazi wa shule</b><br/>Wafanyakazi wataendelea kuwepo eneo la shule.</p> <p>Wafanyakazi wataendelea kusaidiwa kutunza ustawi wao kupitia shule zao na Programu ya Msaada wa Wafanyakazi.</p> <p><b>Wazazi</b><br/>Wazazi wafuate mashauri kutoka shule yao kuhusu protokali za kuacha na kuchukua watoto.</p> | <p>Shughuli za shule za kila mara, kama michezo, kambi na safari zitaanza tena kulingana na kuondoa vizuizi vya usafiri.</p> |

